



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA
CHUO CHA UTUMISHI WA UMMA TANZANIA



TANGAZO LA MAHAFALI

KAIMU AFISA MTENDAJI MKUU NA MKUU WA CHUO CHA UTUMISHI WA UMMA TANZANIA ANAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA **MAHAFALI YA 30** YA CHUO HICHO KWA WANACHUO WALIOHITIMU KATIKA MWAKA WA MASOMO ULIOANZA MACHI 2018 – JANUARI 2019 YATAFANYIKA SIKU YA **IJUMAA, TAREHE 10 MEI 2019** KATIKA TAWI LA MTWARA.

MGENI RASMI ANATARAJIWA KUWA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA.

Wahitimu Wanaotaka Kuhudhuria Mahafali Wanatakiwa Kuzingatia Mambo Yafuatayo:-

1. Kuthibitisha ushiriki kabla ya siku ya **Alhamisi tarehe 09 Mei 2019** kwa namba zifuatazo:-
 - ✓ **Namba za Simu:** 0692461164, 0716708041, 0719953705 na 0789056331
 - ✓ **Email:** graduation@tpscmtwara.ac.tz
2. Gharama za kukodi skafu ni Tsh. 10,000/= (Hairudishwi). Gharama hizi zitalipwa kwa **"Control Number"** ambayo mshiriki ataipata kwa kuwasiliana na Wahasibu kwa namba **0717597780 na 0715376797**. Aidha mshiriki awasilishe uthibitisho wa malipo Ofisi ya Uhasibu kwa ajili ya kupatiwa risiti kabla ya kujaza mkataba wa kukodi skafu.
3. Wahitimu wote wanatakiwa kuvaa suti rangi nyeusi au bluu na mashati meupe
4. Mazoezi kwa wahitimu washiriki (**Rehearsal**) yatafanyika siku ya Alhamisi ya tarehe 09 Mei 2019 saa 8:00 mchana mahali yatakapofanyika Mahafali.
5. Majina ya wahitimu yanapatikana katika tovuti ya chuo: www.tpsc.go.tz, www.tpscmtwara.ac.tz au katika tovuti za Kampasi



LIMETOLEWA NA AFISA MTENDAJI MKUU
CHUO CHA UTUMISHI WA UMMA TANZANIA

